



THE Minister for Livestock and Fisheries Mashimba Ndaki (third left) and Deputy Minister Pauline Gekul (right) inspect goats for slaughtering when they visited Dodoma Slaughterhouse yesterday. Left is Permanent Secretary in the Ministry of Livestock and Fisheries (Livestock), Prof Elisante Ole Gabriel, and other officials. (Photo: Courtesy of the Ministry)

1 DAILY NEWS M, 200

Civil servants challenged to work hard, professionally

From DAILY NEWS
Reporter in Dodoma

MINISTER for Works and
Transport Dr Leonard Ch

3/00025

Ufugaji samaki mabwawani, vizimba kupunguza uvuvi haramu

**Na Mbaraka Kambona,
Dodoma**

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mshamba Ndaki amesema ufugaji wa samaki katika mabwawa na vizimba ukhamasishwa na kupewa maukumo mkubwa utasaidia kuongeza wingi wa samaki na utesaidia kupunguza uvuvi haramu katika maji ya asili.

Ndaki aliyasema hayo alipotembelea shamba la Waziri Mkuu Mstaafu, Mizengo Pinda lilipo jijini Dodoma juzi.

Alisema serikali imefanya kazi kubwa katika kuimarisha sekta ya uvuvi, ikiwemo ufugaji wa samaki katika vizimba na mabwawa lakini alinisitiza kuwa kuna hitajika kuongeza nguvu na jitihada zaidi kuwahamasisha wananchi kujingaza katika ufugaji wa samaki, ili kujiongeza kipato na kupunguza utegemezi wa mazao ya samaki kutoka katika maji ya asili.

"Ufugaji wa samaki kwa kutumia

vizimba na mabwawa, utatusaidia kupunguza purukushani kati ya serikali na wavuvi haramu kwa sababu kama samaki wengi wetapatikana kupitia ufugaji, watu hawataona haja ya kuhangaika na uvuvi usio na tija," alisema Ndaki na akiongeza kuwa:

"Tunahitaji kufanya jitihada zaidi kutangaza na kuhamasisha ufugaji wa samaki hasa kwa kutumia mabwawa ya gharama nafuu kama malambo, ili wafugaji na wananchi kwa ujumla waweze kuona ufugaji huo ni nafuu na wanaweza kupata kipato kupitia kazi hyo".

Aliongeza kuwa hamasa ya ufugaji wa samaki ikiwa kubwa na wanunuzi nao wataongezeka, jambo ambalo litafanya pia kuongezeka kwa wawekezaji katika vyakula na ukuzaji wa vifaranga na hivyo kutatua changamoto iliyopo sasa ya uchache wa vifaranga na vyakula vya samaki.

"Ndani ya Wizara tutaona namna ya kujipanga ili tuendelee

kuiwzesha zaidi hi sekta ya uvuvi iweze kukua zaidi na kuongeza kipato cha watu wetu na kutoa mchango mkubwa katika pato la taifa," alisema.

Awali wakati akimkaribisha Waziri huyo shambani hapo, Pinda alisema changamoto kubwa anayoipata shambani hapo ni kutopatikana kwa urahisi vifaranga vya samaki pamoja na chakula cha uhakika.

"Hapa tunapata changamoto ya vifaranga vya samaki havipatikani kwa urahisi, lakini pia hakuna mahali ambapo unaweza kusema hapa wanazalisha chakula cha uhakika," alisema Pinda.

Aliongeza kuwa pamoja na jitihada kubwa za serikali katika kuimarisha sekta ya uvuvi, lakini angetamani kuona sekta hiyo inaendelea kupewa nafasi kubwa zaidi hasa katika ufugaji wa samaki wa kutumia mabwawa na vizimba, kwani utasaidia wananchi kujipatia kipato na kukuza uchumi wao.

Naye Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Uvuvi) Dkt. Rashid Tamatamah alisema vya sasa serikali inaendelea karabati vituo vya uzalishaji wa vifaranga, ili kuongeza uwemi wa uzalishaji ikiwemo kuimarisha mashamba darasa kwa ajili ya kubandisha watu namna ya kutengeneza chakula cha samaki na ufugaji wa samaki.

Dkt. Tamatamah aliongeza kuwa, serikali inaendelea kuhamasisha uwekezaji katika uzalishaji wa vifaranga na uzalishaji wa chakula na kwa sasa wapo katika mazungumzo na serikali ya Misri, ili kampuni zao ziwaze uwekezaji katika uzalishaji wa vifaranga na vyakula vya samaki hapa nchini.

Ndaki alifanya ziara hii kwa muda mfupi baada ya kuapishwa wakati wa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Desemba 9, mwaka huu. Ziara yake ya kwanza ilikuwa kutamaliza machinjio ya Dodoma na shamba la Pinda.



Katibu Mkuu, Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Uvuvi), Dkt. Rashid Tamatamah (kulia) akimueleza jambo Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dkt. Binilith Mahenge (kushoto) walipotembelea machinjio ya Dodoma juzi, yaliyopo jijini Dodoma. Katikati ni Katibu Mkuu, Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Mifugo), Prof. Ellsante Ole Gabriel. (Na Mpingapicha Wetu) MASHA 11, 2020

KAZI

Wafanyakazi wa machinjio ya Dodoma wakiwa katika hatua za kuwaandaa mbuzi waliochinjwa tayari kwa ajili ya kupelekwa sokoni. Machinjio hayo yana uwezo wa kuchinja ng'ombe 300, mbuzi na kondoo 200 kwa siku. Na Mpigapicha Maalumu



MWANANCHI, DIS 21, 2020